HUKUMU YA ANAEFUNGA HALI YA KUWA HASWALI.

SWAHILI.

IMEANDIWA NA:

DAUDI ABUBAKARI.

IMEPITIWA NA:

ABUBAKARI SHABANI

حكم صوم تارك الصلاة.

اللغة السواحلية.

جمعه وكتبه: داود أبوبكر.

راجعه:

أبوبكر شعبان روكونكوا

بسم الله الرحمن الرحيم

Utangulizi

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, na rehma na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad (s.a.w) na watu wake na Maswahaba wake wote. Amma baad:

Fatawa ya Sheikh Uthaymiyn katika Hukmu ya Mfungaji Saum ambaye Haswali.

Swali:-
Nini Hukmu ya Mtu anaefunga lakini Haswali?

Jibu:-
Mwenye kuacha swala huku anafunga sio Sahih Saumu yake wala Haikubaliki,Kwa hakika mwenye Kuacha Swala ni Kafir Murtad, kwa Kauli ya Allah inayosema

((فإن تابوا وأقاموا الصلاه(ت) وآتوا الزكاه(ت) فإخوانكم فى الدين))
(التوبه : ١١)

Anasema Allah "Wakitubu na Wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka basi hao ni ndugu zenu katika Dini" (Tawbah Aya 11).

Na Kauli ya Mtume (s.a.w) aliposema"Ahadi iliyopo Kati yetu na wao ni Swala na Yeyote atakaeacha Swala amekufuru"
Na akasema tena

(بين الرجل وبين الشرك والكفر ترك الصلاه)

"Kati ya Mtu na Shirk na Kufru ni kuacha Swala"
Na hii ni Kauli ya Jumla ya Maswhaba kwa yule asiyekuwa pamoja nao.

Anasema Abdullah Ibn Shaqiyq (r.a) Naye alikuwa miongoni mwa Tabi'in ambaye ni Maarufu;-"Walikuwa Maswhaba wa Mtume (s.a.w) Hawakuona Kitu ambacho Mtu anaweza kuacha akawa Kafir Kinyume na mwenye Kuacha Swala.
Na kwa hili anapofunga Mtu na hali ya kuwa Haswali Swaumu yake ni yenye Kurudishwa haikubaliki wala Haina manufaa mbele ya Allah siku ya Qiyamah,
Nasisi tunasema: Swala Kisha Saumu na Amma atakaefunga akawa Haswali basi Saumu yake anarejeshewa mwenyewe,Kwa hakika Kafir Haikubaliwi Ibada yake.
Pia Allah amewaandalia adhabu kali wenye kuswali ilihali wanazisahau swala zao, amesema Allah mtukufu :

{ فويل للمصلين الذين هم عن صلاتهم ساهون} (ماعون ٤-٥)
(Basi, ole wao wanao Sali Ambao wanapuuza Sala zao).
Katika hizi aya Allah ameeleza adhabu ambayo watafikia wale ambao wanaswali ila swala zao wanazisahau na kupuuzia mpaka muda wake unapita, sasa ikiwa hali yao nikama hiyo wale wasio swali kabisa hawawezi kuwa waislam.

Tunamuomba Allah atudumishe katika swala na tuwe niwenye kutekeleza swala katika wakati wake.